

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MWANASHERIA MKUU WA
ZANZIBAR KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO KUHUSU
MASUALA YA KISHERIA KATIKA MIKOPO (LEGAL ASPECTS OF
LENDING) KWA MAWAKILI WA SERIKALI ZANZIBAR KATIKA
UKUMBI WA MADINAT AL-BAHR,
TAREHE 16 APRILI, 2026**

**NDUGU SHAABAN RAMADHAN ABDALLA, NAIBU MWANASHERIA
MKUU WA ZANZIBAR;**

**NDUGU PASCAL MIHAYO, MKURUGENZI WA HUDUMA ZA
BIASHARA NA KATIBU WA KAMPUNI CRDB;**

**NDUGU ABDALLAH DUCHI, MENEJA WA BIASHARA CRDB, ZONI
YA ZANZIBAR;**

WAKUFUNZI WETU KUTOKA TAASISI TOFAUTI;

**MAWAKILI WA SERIKALI KUTOKA AFISI YA MWANASHERIA
MKUU NA TAASISI NYENGINE ZA SERIKALI;**

MABIBI NA MABWANA.

ASSALAM ALAYKUM WARAHMATULLAHI WABARAKATUH.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema na katika hali ya amani, kwa lengo la kushiriki katika mafunzo muhimu yanayohusiana na **Masuala ya Kisheria katika Mikopo (Legal Aspects of Lending)** ambayo ni sehemu muhimu ya shughuli za kisheria na kifedha katika utendaji wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, kwa namna ya kipekee, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **CRDB Bank PLC** kwa kufadhili mafunzo haya. Ushirikiano wenu ni kielelezo cha dhamira ya Taasisi za kifedha kushirikiana na Serikali katika kujenga uwezo wa kitaalamu na kuimarisha misingi ya

uwajibikaji na uwazi katika maeneo muhimu yanayohusiana na usimamizi wa mikataba ya kifedha.

NDUGU WASHIRIKI,

Baada ya utangulizi huo mfupi, sasa ni vyema tukajielekeza katika lengo lililotukutanisha hapa ambalo ni mafunzo kuhusiana na Masuala ya Kisheria katika Mikopo (Legal Aspects of Lending), ambayo ni dhana pana sana katika sekta ya Uchumi na Biashara.

Aidha, ni muhimu kutambua kuwa, tofauti na mikopo ya masharti nafuu (Concessional Loans), mikopo ya aina hii (Commercial Loans) huja na vigezo na viwango vya kibiashara vinavyoendana na soko, masharti ya ulipaji yenye ukomo na uwajibikaji mkubwa na mara nyingi huambatana na masharti ya kisheria yenye uzito mkubwa. Kwa mantiki hiyo, mikopo hii huhitaji umakini wa hali ya juu katika maandalizi, majadiliano na utekelezaji wake, ili kuhakikisha kuwa Serikali haiingii katika mikataba itakayopelekea kudumaza uchumi wa nchi kwa muda mrefu.

NDUGU WASHIRIKI,

Ni vyema ikaeleweka kuwa, matumizi ya dhana ya mikataba ya mikopo katika nyanja ya kimataifa, yamekuwa yakiongezeka kwa kasi, hasa katika ufadhili wa miradi mikubwa ya kimbakati. Kwa upande wa Zanzibar na hasa katika Awamu ya Nane ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni dhahiri kuwa kumekuwepo na ongezeko la mahitaji ya rasilimali za kifedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, bandari, viwanja vya ndege na vituo vya afya. Lengo kuu la Serikali likiwa ni kuleta maendeleo kwa kuimarisha miundombinu na huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Katika kukabiliana na mahitaji ya kifedha, Serikali imekuwa ikitumia mbinu mbali mbali za upatikanaji wa fedha, ikiwemo utaratibu wa kupata mikopo ya kibiashara (Commercial Loans).

Mikataba ya aina hii mara nyingi huandaliwa kwa kufuata viwango vya kimataifa na hujumuisha vipengele muhimu ikiwemo Sheria itakayotumika (Governing Law), Utaratibu wa utatuzi wa migogoro hususan kupitia usuluhishi wa kimataifa (International Arbitration), Dhamana za Serikali (Sovereign Guarantees) na mgawanyo wa hatari (Risk Allocation) kati ya wahusika wa mkataba.

Kutokana na upekee huo, ni dhahiri kwamba Mawakili wa Serikali wanapaswa kuwa na uelewa mpana wa sheria za kimataifa, mikataba ya kifedha, pamoja na mbinu za majadiliano (negotiation skills) kwa ajili ya kulinda maslahi ya taifa katika mikataba hii.

NDUGU WASHIRIKI,

Kwa kuwa utaratibu mzima wa kupata mikopo unahusisha Mikataba mikubwa baina ya Serikali na wakopeshaji; hali hii inaweka wajibu mkubwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Mawakili wa Serikali kwa ujumla, kuhakikisha kuwa; Mikataba yote inafanyiwa uchambuzi wa kina wa kisheria kabla ya kutiwa saini kwa ajili ya utekelezaji wake. Aidha, Mawakili wa Serikali wanatakiwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Serikali yanalindwa kikamilifu, kuhakikisha kuwa masharti ya mikataba ni ya haki, wazi na yanayotekelezeka na hatari zote zinazoweza kujitokeza zinatambuliwa mapema na kudhibitiwa ipasavyo.

Ni vyema, pia, tukatambua kuwa makosa madogo katika hatua za awali za mkataba yanaweza kusababisha athari kubwa za kifedha na kisheria kwa Serikali katika siku zijazo.

NDUGU WASHIRIKI,

Mafunzo haya yana umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa kazi za Serikali, lakini pia kwa upande mwingine mafunzo haya yana umuhimu wa kipekee kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kwa Mawakili wa Serikali waliopo katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kuwa yanalenga kuimarisha uwezo wa kitaalamu wa Mawakili wa Serikali katika kushughulikia Mikataba ya Mikopo; kuongeza uelewa wa masuala ya kisheria na kifedha katika ngazi ya kitaifa na kimataifa; kuimarisha uwezo wa kufanya majadiliano (Contract

Negotiation) yenye tija kwa niaba ya Serikali; kuwezesha utambuzi na udhibiti wa hatari (Risks) zinazohusiana na mikataba ya kifedha na kuhakikisha kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu inaendelea kuwa ni nguzo imara katika kushauri na kulinda maslahi ya Serikali.

NDUGU WASHIRIKI,

Kwa kuhitimisha, na kwa kutilia maanani mada zitakazowasilishwa, napenda kusiondaza kuwa maarifa mutakayoyapata katika mafunzo haya ni rasilimali muhimu sana katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku. Hivyo, ni matarajio yangu kuwa mutayatumia kwa ufanisi mkubwa katika kuhakikisha mikataba yote inayohusiana na mikopo inalinda kikamilifu maslahi ya Zanzibar.

Kipekee na kwa mara nyengine tena, napenda kushukuru uongozi wa CRDB Bank PLC kwa mashirikiano yao yaliyopelekea kufanikisha mafunzo haya. Aidha, napenda kuwashukuru wakufunzi wetu kwa utaalamu wao, pamoja na waandaaji kwa juhudi zao kubwa zilizowezesha kufanyika kwa mafunzo haya ya siku mbili.

Baada ya maelezo hayo, napenda kutamka kuwa mafunzo kuhusiana na masuala ya kisheria katika mikopo (Legal Aspects of Lending) kwa Mwakili wa Serikali nimeyafungua rasmi.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.